

MAELEZO YA MHESHIMIWA JAJI (MST) DKT. STEVEN J. BWANA,  
MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA KWENYE HAFLA YA  
KUWAAGA WASTAAFU WA TUME, UKUMBI WA HAZINA,  
DAR ES SALAAM

---

*Mhe. Balozi Hassan Kattanga,  
Katibu Mkuu Kiongozi,*

*Waheshimiwa Makamishna wa Tume,  
Mhe. Balozi (Mst) John M. Haule,  
Mhe. Immaculate P. Ngwale,  
Mhe. Yahaya F. Mbila,  
Mhe. Khadija A. Mbaraka na  
Mhe. Balozi (Mst) Daniel O. Njoolay.*

*Dkt. Laurean Ndumbaro,  
Katibu Mkuu - UTUMISHI*

*Wastaafu mnaoagwa leo,  
Bw. Nyakimura M. Muhoji,  
Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma.*

*Bw. Bambumbile Mwakyanjala,  
Mkurugenzi - Kitengo cha Miongozo, Uwezesaji na Utafiti.*

*Wakuu wa Idara na Vitengo,  
Watumishi wote wa Tume mliopo hapa.*

*Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana.*

**“NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA”**

---

*Mheshimiwa Balazi Hassan Kattanga, Katibu Mkuu Kiongozi*

Awali, kwa niaba ya Tume ninayoiongoza, napenda kukushukuru kwa kukubali mwaliko wetu ili tushiriki pamoja katika hafla hii, tunafahamu una majukumu mazito lakini mwaliko wetu umeupa uzito unaostahili. Nitumie fursa hii, mosi binafsi kukupongeza wewe kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma, hongera sana.

Pili, nachukua fursa hii pia kuishukuru Sekretarieti yetu ya Tume kwa kuja na wazo jema la kuandaa hafla hii, lengo likiwa ni kuwaaga wastaafu wetu, hongereni sana.

*Ndugu Mgeni rasmi,*

Hafla hii ni kwa ajili ya ndugu zetu, wastaafu ambao kwa kweli leo tuna maneno haya ya kusema; **kuwashukuru, kuwapongeza** kwa utumishi wao uliotukuka na ambao umewawezesha kustaafu kwa staha na kwa heshima kubwa na **kuwataki heri**, katika maisha yao baada ya kustaafu.

*Ndugu Mgeni rasmi,*

Tunafahamu Utumishi wa Umma ni Utumishi na wastaafu hawa tunaowaaga leo hii kwa kuangalia wasifu wao ni kielelezo kuwa waliishi vyema utumishi wao. Ni kielelezo kuwa walitekeleza majukumu yao kwa

bidii, uaminifu na uadilifu mkubwa na kwenu ninyi watumishi wa Tume, ambao ni wastaafu watarajiwa mnapaswa kujifunza kutoka kwao .

*Ndugu Mgeni rasmi,*

Pamoja na kujifunza kutoka kwao, naamini mtatoa ushirikiano kwa Viongozi watakaochukua nafasi zao kama ambavyo mlitoa ushirikiano kwa Viongozi hawa wanaostaafu kwa mujibu wa Sheria, lengo likiwa ni kutekeleza majukumu ya Tume kwa ufanisi zaidi na kwa kiwango cha hali ya juu. Ninaamini kuwa kwa ushirikiano na umoja wenu itawasaidia sana katika kuiimarisha Tume kiutendaji na kuifikisha juu zaidi ya ilipo sasa. Hata hivyo, nafahamu kuwa changamoto zipo na zitaendelea kuwepo, niwaombe sana watumishi wa Tume mmuendeleo kutekeleza majukumu yenu wakati changamoto zilizopo zikiendelea kutafutiwa ufumbuzi kadri inavyowezekana.

*Ndugu Mgeni rasmi,*

Mimi na Makamishna, tumefanya kazi na wastaafu hawa kama Sekretarieti ya Tume kwa mafanikio makubwa. Kupitia vikao vyetu vya Tume wastaafu hawa kwa nafasi zao za Uongozi kila mmoja kwa nafasi yake wamekuwa ni msaada mkubwa kwetu kwa kuwezesha kazi zilizowasilishwa mbele yetu kuzitolea uamuzi sahihi, tunawashukuru sana.

*Ndugu Mgeni rasmi,*

Kwa mujibu wa ratiba ya hafla yetu hii, kuna muda umetengwa kwa ajili ya kuwapatia zawadi wastaafu hawa. Natambua zawadi hizi watakazopewa ni ishara ya kuthamini mchango wao mkubwa waliutoa kwa Tume na Serikali kwa ujumla, kwa kazi kubwa walizofanya katika kipindi chote cha utumishi wao.

Ndugu Mgeni rasmi,

Nihitimishe kwa kutoa wito kwa wastaafu wetu kuwa pamoja na kustaafu kwenu tambueni kwamba Tume tutaendelea kuwatumia wakati wowote tutakapowahitaji kwani tunaamini bado mnao mchango mkubwa kwa Tume, hivyo nawaomba mkubali pale mtakapohitajika ili mtumike kwa maslahi mapana ya Taifa.

*Ndugu mgeni rasmi,*

Mwisho, nahitimisha kwa kuwatakia wastaafu hawa Bw. Nyakimura M. Muhoji na Bw. Bambumbile M. Mwakyanjala pamoja na familia zao afya njema na maisha marefu yenye furaha tele.

**Asanteni sana**